**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**MHESHIMIWA DKT. HAROUN ALI SULEIMAN**
**(MBM)**

**AKIWASILISHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**MEI, 2025**

**YALIYOMO**

**SEHEMU YA KWANZA ............................................... 1**

**1.0 UTANGULIZI................................................................ 1**

1.1. Salamu za Pongezi.........................................................1
1.2. Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nane.......................3

**SEHEMU YA PILI.................................................................. 8**
**2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............................................. 8**
2.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025................................................................8
2.2. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..........8
2.3. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ...................................................9

**SEHEMU YA TATU ........................................................ 37**
**3.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ................................................ 37**
3.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026..................................................37
3.2 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026..................................................38
3.3 Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ............................38

**SEHEMU YA NNE ........................................................ 52**
**4.0 SHUKRANI NA HITIMISHO .................................. 52**
4.1 Shukrani.....................................................................52
4.2 Hitimisho ...................................................................52
**5.0 VIAMBATISHO ......................................................... 55**
Kiambatisho Nambari 1a: Makusanyo ya Mapato Julai/ Machi 2024/2025 na Makadirio ya Mwaka 2025/2026 ..............................................55
Kiambatisho Nambari 1b:Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha 2024/2025 ........................................56
Kiambatisho Nambari 1c: Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai/ Machi 2024/2025 ........................................60

Kiambatisho Nambari 2:Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026....................................61
Kiambatisho Nambari 3: Sheria Zilizofanyiwa Mapitio ..........................................................65
Kiambatisho Nambari. 4: Watumishi Walioajiriwa Kuanzia Julai, 2024 Hadi Machi, 2025 ......................65

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

2. **Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa na afya njema pamoja na uwezo wa kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi tukiwa katika hali ya amani na utulivu.

### 1.1. Salamu za Pongezi

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na mahiri tangu alipoanza kuiongoza Zanzibar katika kipindi hiki cha Awamu wa Nane. Nampongeza kwa dhati pia kwa kusimamia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2020/2025, na kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana. Aidha, tunampongeza Mhe. Rais kwa jitihada zake za kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa wananchi tangu alipokabidhiwa madaraka ya kuiongoza Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia maendeleo makubwa katika ukuwaji wa uchumi na kuimarika kwa sekta za afya, elimu, miundombinu, kuimarika kwa huduma za kijamii, kuongezeka kwa uwekezaji, fursa za kiuchumi kwa wananchi, upatikanaji wa haki pamoja na kasi ya vita dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Tunampongeza Mhe. Rais kwa jitihada zake na tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, busara na hekima katika kuiongoza Zanzibar

5. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa mashirikiano anayoyatoa kwa Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza Zanzibar, kudumisha amani na kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

6. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, nampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025, pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza kwa umakini na weledi Baraza hili Tukufu katika kufikia maamuzi mbalimbali yenye manufaa kwa maendeleo ya Zanzibar. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Baraza la Wawakilishi kwa umahiri wao katika kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali na kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma.

8. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini na Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Maryam Thani Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Gando kwa ushauri na miongozo waliyotupa katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Tunawashukuru kwa dhati kwa ushauri wao walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, tunawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa mashirikiano, mawazo na miongozo waliyokuwa wakitupatia katika kipindi chote cha Baraza la 10 ambayo imekuwa chachu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nane.

9. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru wananchi wa Jimbo la Makunduchi, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha katika Baraza lako Tukufu pamoja na kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo katika Jimbo. Aidha, naishukuru familia yangu hususan Mke wangu mpendwa na watoto wangu kwa mashirikiano yao wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Baraza la 10 linahitimisha shughuli zake kwa kipindi cha miaka mitano na tunatarajia kuenda katika Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2025, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Uteuzi wao ni kielelezo cha imani waliyonayo wana CCM kutokana na uwajibikaji na utendaji wao mahiri.

11. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM.

### 1.2. Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nane

12. **Mheshimiwa Spika,** sote tunashuhudia maendeleo ya haraka yaliyopatikana Zanzibar katika sekta mbalimbali kwa kipindi hiki cha kwanza cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane. Mafanikio haya yanatokana na mwelekeo na maono ya Mheshimiwa Rais katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya watu wa Zanzibar.

13. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kwa muhtasari nielezee baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Nane.

### *i. Kuimarika kwa utawala wa sheria na upatikanaji wa haki*

**14. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana ni yafuatayo:-

a. Juhudi kubwa zimefanywa za kuimarisha Muhimili wa Mahkama kwa kuongeza idadi ya Majaji kutoka Majaji wanane mwaka, 2021 hadi kufikia Majaji 14 mwaka, 2025 wakiwemo wanawake 5. Aidha, miundomibunu ya Mahkama inaendelea kuimarishwa kwa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Mahkama za Mikoa na Wilaya-Unguja na Pemba. Juhudi hizi zimekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa haki na kuzisogeza huduma za Mahkama karibu na wananchi.

b. Ofisi imeweza kushirikiana na taasisi mbali mbali katika kupambana na kupunguza kesi za udhalilishaji kutoka kesi 348 kwa mwaka 2023/2024 hadi kesi 292 kwa mwaka 2024/2025. Mafanikio haya ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Vitendo vya Udhalilishaji.

c. Idadi ya wananchi waliopatiwa msaada wa kisheria imeongezeka kutoka 122,149 (wanawake 65,498 wanaume 56,651) mwaka 2020 hadi 419,401 (wanawake 226,172 wanaume 193,229) mwaka 2023. Aidha, idadi ya watoaji Msaada wa Kisheria imeongezeka kutoka 117 mwaka 2020 hadi 278 mwaka 2024. Juhudi pia zimechukuliwa za kuwawezesha watoaji wa msaada wa kisheria ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwemo usafiri, vishikwambi, printa na laptop.

d. Kupitia Kituo cha Sheria na Utafiti, Ofisi imeweza kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 119 kwa mwaka 2023/2024 hadi wanafunzi 155 kwa mwaka 2024/2025.

e. Ofisi imefanikisha kuanzishwa kwa Skuli ya Sheria, sambamba na mitaala na miongozo mbali mbali ya kitaaluma. Jumla ya Mawakili 96 wamemaliza masomo

yao, 32 wanaendelea na masomo. Aidha, wasaidizi wa sheria 300 wamepatiwa mafunzo.

f. Sheria mbalimbali zenye mnasaba na udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu zimefanyiwa mapitio. Hatua hii imeifanya Tanzania kuendelea kuchukua hatua ya kutekeleza masharti ya kimataifa ya kukabiliana na utakatishaji wa fedha haramu.

g. Kuendelezwa kwa mafunzo ya ndoa ikiwa ni moja ya Mkakati wa Kupunguza Talaka ambazo zimekuwa ni chanzo cha matatizo mengi yanayowapata watoto katika jamii. Jumla ya wananchi 4,722 (wanawake 3,082 wanaume 1,640) wamefaidika na mafunzo ya ndoa tangu yalipoanzishwa.

***ii. Mageuzi katika Sekta ya Utumishi wa Umma***

**15. Mheshimiwa Spika,** Mageuzi makubwa yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma ni: -

a. Ofisi imeimarisha matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki ya Utoaji wa huduma za Utumishi wa Umma, miongoni mwao ni Mfumo wa Maombi ya Ajira (Zan-Ajira), Mfumo wa Masjala ya Kieletroniki (e- Office) na Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (Human Resource and Payroll Management Information System - HR-PayMIS. Aidha, jitihada zinaendelea katika kutayarisha mifumo zaidi ya kiutumishi ikiwemo Mfumo wa Tathmini ya utendajikazi wa Watumishi wa Umma.

b. Ofisi imefanikiwa kuimarisha Maslahi ya Watumishi ikihusisha mishahara na maposho.

c. Serikali imeanza kutumia Miundo ya Utumishi (Scheme of Service) ambapo inawezesha Watumishi kupandishwa vyeo na madaraja. Hatua hii imeondoa malalamiko ya muda mrefu ya watumishi wa umma ya kutozingatiwa ipasavyo uzoefu wao na kupelekea watumishi wakongwe na wapya kupokea viwango sawa vya mishahara.

d. Ofisi imeweza kuidhinisha Miundo ya Wizara, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea. Hatua hii imewezesha kuwepo kwa mgawanyo mzuri wa divisheni na majukumu pamoja na kuongeza ufanisi na tija katika utendaji na utoaji wa huduma.

***iii. Kuimarika kwa Utawala Bora***

**16. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana ni yafuatayo:

a. Kuendelea kufanya ukaguzi wa njia za kisasa kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali na kuongezeka kwa uwazi juu ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa kuanza utaratibu wa Ripoti za Mkaguzi kuwasilishwa kwa uwazi.

b. Ofisi ya Mdhibiti na Mkagzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanikiwa kuanzisha Maabaara ya Kisasa ya Uchunguzi (Forensic Lab) yenye vifaa vya kisasa vya ukaguzi. Hatua hii itawezesha Ofisi ya Mdhibiti kuongeza ubora na usahihi wa ukaguzi unaofanyika.

c. Mabadiliko makubwa ya kisheria na kiumuundo yamefanyika katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi hali iliyopelekea Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na kufanikiwa kuokoa fedha nyingi za Serikali na wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Jumla ya fedha za Serikali **Sh. 4,181,564,509** zimeokolewa. Aidha, Mamlaka pia imenunua vifaa vya kisasa ikiwa ni hatua ya kuanzisha Maabara ya Kisasa ya Uchunguzi (Forensic Lab). Maabara hii ikikamilika itaweza kutumiwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya.

d. Kuanzishwa kwa Televisheni Mtandao (UB Online TV) ambayo inapatikana kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo Youtube, X, Tiktok na Istagram, kwa lengo la kuongeza

upeo wa usambazaji wa taarifa za Taasisi zilizo chini ya Ofisi sambamba na kutoa elimu kwa Umma.

17. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mpango wa Bajeti ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia mafungu ya bajeti 11 yaliyotekelezwa kupitia Programu kuu 14 ambazo zinatekelezwa na Idara na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Ofisi. Utekelezaji wa bajeti wa kila Programu unaelezwa kwa kina katika sehemu zinazofuatia za taarifa hii.

### 2.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

19. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 OR-KSUUB kupitia Taasisi zilizo chini yake ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Sh. 5,592,465,000** ukilinganisha na **Sh. 4,535,900,000** ilizokadiriwa mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la **Sh. 1,056,565,000 (asilimia 23 ya ongezeko).**

20. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2025, **Sh. 2,270,892,852** zimekusanywa sawa na asilimia 41 ya makadirio. Makusanyo haya yanatokana na vyanzo mbalimbali kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1a.**

### 2.2. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

21. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ilipangiwa kutumia **Sh. Bilioni 121,778,058,820** kati ya hizo, **Sh. 64,174,200,036** kwa matumizi ya kazi za kawaida, mishahara na ruzuku na **Sh. 56,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ikiwemo ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya, utayarishaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi na Utekelezaji wa Programu ya

Mageuzi ya Sheria na Utumishi wa Umma. Ofisi pia ilipangiwa kutumia **Sh. 1,516,858,784** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, **Sh. 87,000,000** ni ruzuku kwa wahisani kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF)

22. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 60,063,002,526** zimepatikana **(sawa na asilimia 49 ya lengo).** Kati ya fedha hizo, **Sh.39,530,924,164 (sawa na asilimia 62 ya lengo)** zilitumika kwa matumizi ya kazi za kawaida, mishahara na ruzuku na **Sh. 19,895,828,111 (sawa na asilimia 36 ya lengo)** zilitumika katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Mendeleo, **Sh. 700,000,314 (sawa na asilimia 46 ya lengo)** zimepatikana **(Kiambatisho Nambari 1b na 1c).**

### 2.3. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

23. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, OR-KSUUB ilitekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Urithishaji Viongozi (Succession Plan);

ii. Kuendeleza matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Utumishi wa Umma;

iii. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali;

iv. Kuendelea kuongeza uwelewa kwa jamii juu ya masuala ya msaada wa kisheria;

v. Kusimamia misingi ya utawala bora, maadili na kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumi uchumi; na

vi. Kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa rasilimali za Umma.

24. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji wa Bajeti na matumizi halisi kwa kila Fungu na Programu zilizomo katika Ofisi hii ni kama ifuatavyo:-

### *2.3.1. Fungu G01: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*

25. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G01 linahusisha Programu nne ambazo ni

#### *(i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria*

26. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Kampeni ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia imefanyika katika Shehia za Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Kaskazini Pemba, wananchi 1,246 (wanawake 930 na wanaume 316) wamepatiwa huduma za msaada wa kisheria;

ii. Mafunzo ya haki za binadamu yametolewa kuhusiana na haki za watoto na kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji kwa Madrasa tatu (3) za Wilaya ya Magharibi A - Unguja. Wanafunzi 408 wamepatiwa mafunzo hayo (wanaume 157 na wanawake 251);

iii. Malalamiko 17 yamewasilishwa na wananchi wakiomba kupatiwa huduma za msaada wa kisheria. Malamiko 11 kati ya hayo yanahusiana na hati za ardhi na malalamiko sita (6) yanahusiana na masuala ya kijamii; ikiwemo kufukuzwa kazi kinyume na utaratibu, udanganyifu katika masuala ya fedha; migogoro ya ardhi, wizi na madai ya talaka. Malalamiko mawili yamepatiwa ufumbuzi, manne yamehamishiwa katika taasisi zinazohusika na malalamiko husika na malalamiko matano yanaendelea kufanyiwa kazi; na

iv. Vipindi 20 vya redio vimerushwa hewani Unguja na Pemba, ambapo elimu kuhusiana na taratibu za kupata msaada wa kisheria katika masuala ya mikataba, migogoro ya ardhi, kuripoti vitendo vya udhalilishaji imetolewa pamoja na elimu juu ya jukumu la mwanamme katika malezi.

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu hii ilipangiwa **Sh. 322,791,520** (mishahara **Sh. 202,791,520** na matumizi mengineyo **Sh. 120,000,000).** Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 164,014,548 (sawa na asilimia 51 ya lengo)** zimepatikana ambapo **Sh. 127,571,832** zilitumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 63 ya lengo)** na **Sh. 36,442,716 (sawa na asilimia 30 ya lengo)** zilitumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nambari 1b).**

***(ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora***

28. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala Bora. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Ujenzi umefanyika wa Studio ya kisasa ya Utawala Bora (UB Online TV) ambapo hivi sasa imeanza kutumika. Jumla ya vipindi 47 vinavyohusiana na changamoto mbali mbali za kijamii vimerushwa hewani. Aidha, watendaji wa UB TV wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utangazaji na uendeshaji wa TV hiyo;

ii. Elimu juu ya masuala ya utawala bora imetolewa kwa wananchi waliotembelea Banda la Utawala Bora katika Maonesho ya Kuadhimisha Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe- Pemba. Jumla ya Wananchi 333 walifaidika na elimu hiyo; na

iii. Idara imeendelea kupokea kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Miongoni mwa kero zilizoshughulikiwa ni tatizo la kuharibika kwa miundombinu ya maji katika shehia mbalimbali na kufanikisha kupatiwa ufumbuzi wa tatizo hilo kupitia taasisi husika.

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu hii ilipangiwa **Sh. 303,368,720** (mishahara **Sh. 184,168,720 na Sh. 119,200,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 144,545,375** zimepatikana **(sawa na asilimia 48 ya lengo)** ambapo **Sh. 120,755,325** zilitumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 66 ya lengo)** na **Sh. 23,790,050** zilitumika kwa matumzi mengineyo **(sawa na asilimia 20 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

### *(iii) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*

30. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

31. **Mheshimiwa Spika,** kazi zifuatazo zimetekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji: -

i. Idara imeendelea kusimamia masuala ya kiutumishi, uwajibikaji na maslahi ya watumishi, kwa kuwapatia watumishi likizo, posho mbalimbali na mafunzo. Watumishi 110 wamepatiwa stahiki na fursa mbali mbali ikiwemo likizo (watumishi 57), posho mbali mbali (watumishi 49) na watumishi wanne wamelipiwa gharama za mafunzo ya muda mrefu na mfupi; na

ii. Habari zimeendelea kutolewa kupitia vyombo mbali mbali vikiwemo Televisheni, Radio na Mitandao ya kijamii ili kuwapatia habari wananchi juu ya shughuli zinazotekelezwa sambamba na utoaji wa elimu wa masuala ya Kiutumishi na Utawala Bora.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ilipangiwa kutumia **Sh. 3,388,050,196** (mishahara **Sh. 1,838,050,196** na matumizi mengineyo **Sh. 1,550,000,000).** Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 1,919,395,260** zilipatikana **(sawa na asilimia 57 ya lengo)** kati ya hizo **Sh. 1,273,200,331** zilitumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 69 ya lengo)** na

**Sh. 646,194,929** zilitumika kwa uendeshaji wa Ofisi **(sawa na asilimia 42 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, kazi zifuatazo zimetekelezwa: -

    i. Idara imeratibu kazi mbali mbali za Ofisi zikiwemo: Ripoti za Utekelezaji wa Kazi za Ofisi na vikao vya mashirikiano. Vikao viwili vya mashirikiano vimefanyika kati ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya SMZ na Wizara ya Katiba na Sheria ya SJMT. Kikao cha ngazi ya wataalamu kilifanyika tarehe 17-18 Disemba, 2024 na kikao cha ngazi ya Makatibu Wakuu kilifanyika tarehe 19 Disemba, 2024. Aidha, Idara vile vile iliratibu vikao vya mashirikiano baina Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya SMZ na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya SJMT. Kikao cha ngazi ya wataalamu kilifanyika tarehe 5 Januari, 2025, Kikao cha ngazi ya Makatibu Wakuu kilifanyika tarehe 6 Januari, 2025 na kikao cha ngazi ya Mawaziri kilifanyika tarehe 7 Januari, 2025. Lengo la vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu;

    ii. Takwimu za Viongozi wa Wizara na Taasisi za Serikali zimekusanywa kwa kipindi cha Juni, 2024 pamoja na kukusanya takwimu za Ajira na Mapato ya Ofisi;

    iii. Vikao vyaa Tathmini ya Muda wa Kati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP Midterm Evaluation) kimefanyika kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ili kuona kwa kiasi gani Ofisi imetekeleza mpango huo; na

    iv. Programu na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Ofisi kwa kushirikiana na Washirika wa maendeleo imesimamiwa na kuratibiwa.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ilipangiwa **Sh. 400,376,480 (Sh. 250,376,480**

mishahara na **Sh. 150,000,000 matumizi mengineyo).** Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 201,561,364** zimepatikana **(sawa na asilimia 50 ya lengo),** ambapo **Sh. 165,935,121** ni mishahara **(sawa na asilimia 66 ya lengo)** na **Sh. 35,626,243** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 24 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

***Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

35. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini ya Ofisi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo ifuatayo:-

***a) Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria Awamu ya Pili (LEAP II)***

36. **Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kupitia Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Chuo Cha Mafunzo na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria na umejikita katika kusaidia kujenga uwezo wa Sekta ya Sheria na upatikanaji wa haki kwa wananchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mradi ulitumia **Sh. 401,168,800 (sawa na asilimia 26 ya lengo)** na kazi zilizotekelezwa ni: -

i. Muongozo wa kufundishia (Training Manual) umetayarishwa na umeanza kutumika rasmi Januari, 2025 kwa Mwaka wa Masomo 2025 – 2026;

ii. Kitengo cha Kusaidia Kulinda Waathirika na Mashahidi kiliopo Pemba kimepatiwa vifaa vya TEHAMA ikiwemo Desktop 4, laptop 2 na fotokopi 1;

iii. Jukwaa la Mawakili na Maafisa Sheria limefanyika (wanawake 32 na wanaume 38) kwa lengo la kuwakutanisha mawakili na maafisa sheria na kujadili mafanikio na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao na Mikakati ya kuimarisha Sekta ya Sheria Zanzibar; na

iv. Jukwaa la Nne la Msaada wa Kisheria limefanyika na wadau wa sheria 140 (wanawake 55 na wanaume 85) wameshiriki.

***b) Mradi wa Utoaji wa Haki kwa Kuzingatia Jinsia ili Kuwasaidia Wanawake Kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar***

**37. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Mradi umejikita katika kuwajengea uwezo wanawake ili kukabiliana na kesi za ukatili wa kijinsia. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 **Sh. 298,831,514** zilitumika na kazi zilizotekelezwa ni:-

i. Rasimu ya Muongozo wa Jukwaa la Kitaifa la Haki za Wanawake na Wasichana imetayarishwa na mikutano miwili ya wahusika imefanyika kwa ajili ya kukusanya maoni. Washiriki 45 walihudhuria kwa upande wa Unguja (wanawake 30 na wanaume 15) na Pemba washiriki 90 walihudhuria (wanawake 60 na wanaume 30). Madhumuni ya Muongozo huu ni kutatua changamoto za wanawake na wasichana katika ushirikishwaji wa migogoro ya ardhi na maamuzi katika jamii;

ii. Mafunzo juu ya ushiriki wa wanaume katika malezi; Kanuni elekezi na Mifumo ya Usimamizi wa Familia katika Sheria; na Umuhimu wa Mawasiliano katika Malezi ya Watoto yamefanyika. Wanajamii 40 walishiriki mafunzo hayo wakiwemo wanawake 19 na wanaume 21;

iii. Utafiti kuhusiana na ukatili wa kijinsia (Gender Based Violence) umefanyika na ripoti ya utafiti huo imezinduliwa tarehe 19 Machi, 2025; na

iv. Mafunzo juu ya kukabiliana na kuzuia udhalilishaji wa kijinsia yalitolewa kwa wanafunzi (wanawake 55 wanaume 35) katika Skuli za Sekondari 5 kwa upande wa Unguja na Pemba 4.

***c) Mradi wa Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT).***

38. **Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni wa miezi 15 utekelezaji wake unazihusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahkama Kuu Zanzibar, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mrajis wa Taasisi zisizo za Kiserekali, Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara, Jeshi la Polisi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 **Sh. 3,572,849,786** zilitumika na kazi zilizotekelezwa ni:-

i. Kanuni juu ya upokeaji wa ushahidi wa kielektroniki zimeandaliwa na mafunzo kuhusiana na makosa ya utakatishaji wa fedha haramu yametolewa kwa Majaji, Mahakimu na Makadhi;

ii. Mafunzo yanayohusiana na ushahidi wa kielektroniki katika kuthibitisha makosa ya rushwa, uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha haramu yametolewa kwa Waendesha Mashtaka na taasisi za haki jinai. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza umahiri wa waendesha mashtaka katika kushughulikia uendeshaji wa mashtaka ambayo ushahidi wake ni wa kielektroniki; na

iii. Wakaguzi wa kiuchunguzi 10 na wakaguzi wa fedha watano (5) wamepatiwa mafunzo juu ya kutumia vifaa vya kiuchunguzi vilivyonunuliwa kupitia mradi wa BSAAT.

***Ofisi Kuu Pemba***

39. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Ofisi ilisimamia uratibu wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba ambapo mikutano na ziara za

kutembelea Wizara 17 pamoja na taasisi 9 za Serikali zimefanyika kwa lengo la kufanya ukaguzi wa OPF za watumishi, kuangalia utekelezaji wa miundo ya taasisi pamoja na utekelezaji wa utoaji wa Mkataba wa huduma kwa umma (wateja). Pia kutoa maelekezo ya kiutumishi kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Utumishi; na

ii. Kuratibu na kufanya vikao 6 vya watumishi kwa maafisa 37 wa Wizara na taasisi za SMZ Pemba kwa lengo la kuzungumzia nidhamu na uwajibikaji kazini.

**40. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi Kuu Pemba imepangiwa kutumia **Sh. 625,072,800.** Hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizopatikana ni **Sh. 361,541,902 (sawa na asilimia 56 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

***(iv) Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma***

**41. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi na Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi.

***Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi***

**42. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

i. Idara imesimamia utoaji wa vibali 25 na nafasi 6,625 zimeajiriwa ili kujaza nafasi tupu katika Taasisi za Umma kwa mwaka Fedha 2024/2025;

ii. Mafunzo juu ya Uandaaji wa Mahitaji ya Mafunzo yametolewa kwa taasisi 18 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jumla ya watumishi 1,113 wamejumuishwa katika Mpango wa Mafunzo wa miaka 5;

iii. Idara imeratibu mafunzo kwa watumishi na watumishi 989 wamepata nafasi za mafunzo katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi wakijiendeleza kimasomo;

iv. Idara imeratibu mafunzo ya muda mrefu yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo ambapo jumla ya watumishi 8 wamepata mafunzo ya muda mrefu na maombi 25 yamefanyiwa uchambuzi kwa mwaka wa masomo 2025/2026 na kuwasilishwa katika Ofisi za KOICA Tanzania. Watumishi 20 wamechanguliwa kushiriki katika Mafunzo ya muda Mrefu nchini China,watumishi 5 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo ya muda mrefu kwa njia ya mtandao (Online)katika ngazi ya Shahada ya Uzamili (Master) nchini Uingereza. Aidha, watumishi 35 walichaguliwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi nchini India, watumishi 4 walishiriki mafunzo ya muda mrefu nchini Japani na muda mfupi mmoja (1) na watumishi 6 wamechaguliwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi nchini MISRI;

v. Zoezi la uhakiki wa watumishi limefanyika kwa upande wa Unguja na watumishi ambao hawafanyii kazi kwa mujibu wa fani walizosomea, wamepangwa na wengine wamepangiwa katika Taasisi zenye upungufu wa watumishi; na

vi. Idara imetoa matoleo mbali mbali yakiwemo Urithishwaji Viongozi (succession Plan) unaozingatia kukaimu nafasi katika Taasisi za Umma, kipimo cha madawa ya kulevya kwa watumishi wapya, kuacha Kazi kwa watumishi wenye Mikopo, Utaratibu wa watumishi kwenda na kurudi likizo bila ya Malipo na matumizi ya Simu na Mitandao ya Kijamii wakati wa Saa za Kazi.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu kwa upande wa Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi ilipangiwa kutumia **Sh. 841,471,120 (Sh. 451,471,120** mishahara na **Sh. 390,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 414,171,555** zimepatikana **(sawa na asilimia 49 ya lengo)** ambapo **Sh. 334,575,295** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 74 ya lengo) na Sh. 79,596,260** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 20 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

### *Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi*

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Miundo 87 ya Taasisi, Mashirika, Mamlaka, Kampuni, Wakala na Taasisi zinazojitegemea za SMZ imefanyiwa mapitio kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kupunguza ukubwa wa Miundo ya Taasisi pamoja na gharama za uendeshaji wa Taasisi hizo. Ripoti ya mapitio hayo imekamilika na itawasilishwa Serikalini kwa maamuzi;

ii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Utumishi katika Taasisi za Umma umefanyika sambamba na mapitio ya Miundo ya Utumishi kwa Wizara 18 ili kuongeza kada mbali mbali ambazo hazikuwepo na kuongeza Madaraja ya kiutumishi kutoka matano (5) hadi madaraja sita (6) na kuongeza muda wa mtumishi kuweza kulitumikia daraja moja kutoka utaratibu miaka mitatu (3) kwa sasa hadi kufikia minne (4) kwa kila kada;

iii. Maandalizi ya Mifumo ya Kupima Utendajikazi wa Watumishi wa Umma (Public Employee Performance Management Information System-PEPMIS) yanaendelea. Aidha, Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (HR–PayMIS) umeanza kufanya kazi na maslahi ya watumishi wote wanaolipwa kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wameanza kulipwa kwa kutumia mfumo huo kuanzia mwezi Februari, 2025. Mfumo huu unarahisisha upatikanaji wa taarifa za Watumishi na Malipo ya stahiki za Watumishi, sambamba na kutatua changamoto ya watumishi hewa na watumishi kulipwa malipo na viwango vya mishahara wasivyostahiki;

iv. Ushauri wa kitaalamu umetolewa kwa Miundo 14 ya Taasisi za Serikali. Miundo hiyo ni;- Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar; Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Bahari Zanzibar (ZAFIRI); Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar; Kampuni ya Bima ya Takaful Zanzibar;

Taasisi za Uhasibu; Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar; Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar, Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Tume ya Idara Maalum za SMZ; Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar; Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Baraza la Kiswahili Zanzibar;

v. Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Umma umekamilika na mafunzo yametolewa juu ya utekelezaji wake. Muongozo huo tayari umewekwa katika tovuti ya Wizara kwa ajili ya Taasisi za Umma kuweza kuutumia kama ilivyokusudiwa;

vi. Uhakiki wa Mishahara pamoja na vyeti vya taaluma umefanyika kwa watumishi wa Vikosi Maalumu vya SMZ, na marekebisho ya maslahi yao yataanza katika mwaka mpya wa fedha;

vii. Matayarisho ya Mkataba wa Utendaji kazi (Performance Contract) yamekamilika na Mkataba huo unatarajiwa kuanza kutumika kwa majaribio kwa baadhi ya Taasisi kwa mwaka mmoja kabla ya kuanza kutumika katika Wizara na Taasisi zote za Serikali. Lengo la kuanzishwa kwa mkataba huu ni kupima uwajibikaji wa Viongozi na kuweka utaratibu maalum wa kutathmini viongozi kuhusu utendaji na matunda ya juhudi zao; na

viii. Tathmini ya uwezo wa kifedha kwa Taasisi 26 zinazopokea Ruzuku umefanyika ili kuangalia uwezekano wa kujitegemea katika gharama za uendeshaji na kutoa gawio Serikalini. Mapendekezo ya Taasisi zenye uwezo huo yamewasilishwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa utekelezaji.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi imepangiwa kutumia **Sh. 848,569,200 (Sh. 648,569,200** mishahara na **Sh. 200,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 553,737,574** zimepatikana **(sawa na asilimia 63 ya lengo)** ambapo **Sh.**

**504,489,114** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 78 ya lengo)** na **Sh. 34,239,460** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 17 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

***Taasisi Zinazopokea Ruzuku***

**46. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 OR-KSUUB imesimamia ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Chuo cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Taasisi hizi zimetekeleza mambo yafuatayo: -

***a)Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)***

**47. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utawala wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kimetekeleza kazi zifuatazo:

i. Mafunzo elekezi kwa watumishi wapya 761 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma yamefanyika Unguja na Pemba;

ii. Watumishi wa Umma 331 kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali wamepatiwa mafunzo ya kujenga uwezo;

iii. Wastaafu watarajiwa 91 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma wamepatiwa mafunzo;

iv. Wanafunzi 1,720 (Watumishi wa Umma 344 na Wananchi wengine 1,376) wamesajiliwa kwa masomo ya ngazi ya Shahada, Astashahada na Shahada ya Kwanza;

v. Watumishi 10 wamepatiwa fursa ya mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao, 3 Shahada ya Kwanza na 7 Shahada ya Uzamili. Aidha, watumishi 83 wamepatiwa mafunzo ya kitaalamu katika fani mbalimbali; na

vi. Mashirikiano ya Chuo na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya Nchi yanaendelea yakiwemo Chuo cha Utumishi wa Umma Magogoni (TPSC), Chuo Kikuu cha Diplomasia Kurasini (CFR), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) pamoja na Kenya School of Government (KSG).

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Chuo kilipangiwa ruzuku ya **Sh. 3,191,100,000** kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 2,263,071,202** zimepatikana. **(sawa na asilimia 71 ya lengo)** Aidha, Chuo kilipangiwa kukusanya **Sh. 3,243,805,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na kimefanikiwa kukusanya **Sh. 1,412,834,842 (sawa na asilimia 44 ya makadirio).**

***b) Skuli ya Sheria Zanzibar***

49. **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kilitekeleza kazi zifuatazo:-

i. Waombaji 44 wamejiunga na Skuli ya Sheria. Kati ya hao, 34 ngazi ya Mawakili na 10 kwa Programu ya Mavakili;

ii. Skuli ya Sheria imeanzisha Mafunzo ya Mavakili kwa wanafunzi 15 wa Kundi la Kwanza la Skuli ya Sheria;

iii. Skuli imewezesha wanafunzi wa kundi la kwanza la Mavakili kufanya Mitihani ya uandishi (Written Practical Exams - WPE) na kujipima uwezo binafsi (ICA) ambapo jumla ya wanafunzi 15 wamefanya mitihani hio;

iv. Kanuni za Mitihani za Skuli ya Sheria zimeandaliwa na kutumika rasmi kwa wanafunzi wa mwaka wa masomo 2025 – 2026 kwa Programu ya Mawakili pamoja na Programu ya Vakili; na

v. Mafunzo ya vitendo (Field Attachment) yamefanyika kwa wanafunzi 28 katika awamu mbili tofauti.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Skuli ya Sheria ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Sh. 1,010,200,000.** Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 720,923,071 (sawa na asilimia 71 ya lengo)** zimepatikana. Aidha, Skuli ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Sh. 179,500,000,** hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 60,340,000 (sawa na asilimia 34 ya makadirio)** zimekusanywa.

### *2.3.2. Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki*

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mahkama Kuu-Zanzibar na kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kazi zifuatazo zimetekelezwa: -

i. Mahkama imepokea na kufanyia kazi mashauri mbalimbali yaliyopokelewa kama inavyoonekana katika jadueli:

| MAHKAMA/AINA YA MASHAURI | MASHAURI YALIYOPOKELEWA | MASHAURI YALIYOTOLEWA MAAMUZI | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| MAHKAMA YA ZANZIBAR | 9,106 | 6,590 | 72 |
| JINAI | 2,364 | 1,671 | 71 |
| MADAI | 1,658 | 940 | 57 |
| UDHALILISHAJI | 292 | 179 | 61 |
| KADHI | 4,531 | 3,668 | 81 |
| MADAWA YA KULEVYA | 165 | 73 | 44 |
| MAHKAMA YA WATOTO | 96 | 59 | 61 |

ii. Mahkama imeratibu vikao viwili vya ushirikiano na wahusika wa haki jinai kwa lengo la kuharakisha mienendo ya kesi;

iii. Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yamefanyika tarehe 10/02/2025 Mgeni rasmi alikua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kauli mbiu ni; - ***"Utawala wa Sheria ndio Msingi wa Haki, Amani na Maendeleo katika Jamii";***

iv. Mahkama ya Zanzibar inatekeleza Mradi wa Maboresho ya Mahkama (Zi-JUMP) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi huu una lengo la Kuboresha ufikiaji, ufanisi, na uwazi wa huduma za Mahkama kwa wananchi kwa maeneo makuu matatu (Upatikanaji wa Haki, Ufanisi wa Mahkama na Ushirikishwaji wa wahusika na wananchi Mahkamani). Vile vile, Mradi wa Zi-JUMP utaelekeza nguvu katika kuimarisha miundombinu ya Mahkama,

kuongeza taaluma kwa wafanyakazi wa Mahkama, kuandaa Mkakati wa Kijinsia Mahkamani, kupunguza mrundikano wa mashauri na kuongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi; na

v. Mafunzo mbalimbali ya kukutanisha na wahusika wa Mahkama za Watoto yamefanyika kwa kushirikiana na Shirika la Watoto Duniani, ambapo vifaa vya Tehama vimenunuliwa ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha upatikanaji wa haki ya mtoto Mahkama ya Zanzibar.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mahkama Kuu ilipangiwa kutumia **Sh. 68,900,700,000 (Sh. 7,462,900,000** mishahara na **Sh. 3,767,600,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2025, **Sh. 9,183,176,901** zimepatikana **(sawa na asilimia 74 ya lengo)** ambapo **Sh**. **6,718,072,350** zilitumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 86 ya lengo)** na **Sh. 2,465,104,551** zilitumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 54 ya lengo).**

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mahkama ilipangiwa bajeti ya **Sh. 25,500,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mkoa na Wilaya na **Sh. 500,000,000** kwa Mradi wa Mifumo ya Kielektroniki. Hadi kufikia Machi 2025, **Sh.11,968,435,561** zimepatika katika Mradi wa Ujenzi wa Mahkama **(sawa na asilimia 36 ya lengo).** Aidha, Mradi wa Maboresho ya Mahkama (Zi-JUMP) imepangiwa **Sh. 28,500,000,000.** Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 7,821,652,550** zimepatikana **(sawa na asilimia 27 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b na 1c).**

54. **Mheshimiwa Spika,** Mahkama ya Kadhi, ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Sh. 1,964,700,000** hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 1,647,467,508 (sawa na asilimia 84 ya lengo)** zimepatikana ambapo **Sh. 1,248,467,424** zilitumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 84 ya lengo) na Sh. 399,000,000** zilitumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 83 ya lengo).**

**55. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mahkama ilikadiriwa kukusanya **Sh. 1,239,894,000** hadi Machi 2025, **Sh. 297,934,829** zimekusanywa **(sawa na asilimia 24 ya makadirio).**

### *2.3.3.Fungu G03: Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria*

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Ofisi imetekeleza shughuli zifuatazo;-

i. Miswada Mitatu na Kanuni 10 za Sheria tofauti zimetayarishwa kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi;

ii. Matangazo 54 ya Kisheria yametayarishwa na kuwasilishwa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

iii. Mikataba 993 imetolewa ushauri, kati ya hiyo, 689 ya Bidhaa na Huduma, 154 ya Ujenzi, 128 ya Ushauri Elekezi na 22 Kodi (Lease);

iv. Hati za Maelewano (MoU) 177 zimetolewa ushauri wa kisheria katika sekta ya Elimu, Uchumi, Usafiri, Utalii, Makaazi, Afya, Ardhi, Ujenzi, Teknolojia, Kilimo, Utamaduni, Sheria, Mazingira na Fedha;

v. Ofisi iliendelea kuiwakilisha Serikali kwenye Mashauri ya Kesi za Madai na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo, kesi 20 zimefunguliwa mahkamani. Aidha kesi Saba (7) zilisikilizwa na zilimalizika, ambapo Kesi sita (6) Serikali ilishinda na kesi moja (1) Serikali ilikata rufaa; na

vi. Sheria nane 8 zimefanyiwa mapitio na zipo katika hatua mbali mbali za utafiti. Maeneo ya utafiti ni pamoja na:

   a. Sheria ya Utumishi wa Umma Nam.2 ya Mwaka 2011 katika eneo la upandishaji cheo (promotion) kwa watumishi wa umma;

   b. Sheria ya Mahusiano Kazini Nam.1 ya Mwaka 2005 katika eneo la utatuzi wa migogoro ya wafanyakazi wa

sekta binafsi, eneo la biashara (kuangalia masuala ya wingi wa leseni na vibali kwa wafanyabiashara);

c. Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam.12 ya Mwaka 1992;

d. Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam.10 ya Mwaka 1990 katika eneo la umiliki na usajili wa ardhi;

e. Sheria ya Mipango Miji na Vijiji Sura ya 85 ya Mwaka 1955 katika eneo la mipango miji;

f. Sheria ya Maji Nam.4 ya Mwaka 2006 katika eneo la huduma na upatikanaji wa maji nchini;

g. Sheria ya Umeme Nam.3 ya Mwaka 2006 katika eneo la huduma na upatikanaji wa umeme nchini; na

h. Sheria ya Uchaguzi Nam.4 ya Mwaka 2018 katika eneo la uchaguzi.

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 5,912,100,000 (Sh. 3,543,100,000** mishahara na **Sh. 2,369,000,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2025, **Sh. 3,551,115,071** zimepatikana **(sawa na asilimia 60 ya lengo)** ambapo **Sh. 2,598,688,743** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 73 ya lengo)** na **Sh. 952,426,328** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 40 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

### *2.3.4. Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai*

58. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Majalada ya kesi 2,850 ya makosa mbali mbali ya jinai yamepokelewa na kutolewa maamuzi: 469 Udhalilishaji; 45 Makosa ya Dawa za Kulevya; 25 makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; 1,032 makosa ya wizi; 304 Uvunjifu wa Amani; 571 makosa ya Shambulio; 70 makosa ya Usalama Barabarani; 30 mauaji na mengineyo 304;

ii. Kesi 1,137 zimefunguliwa katika Mahkama za Mikoa na Mahkama za Wilaya ambapo kesi 606 zimepatikana na hatia, kesi 272 watuhumiwa wameachiliwa huru, na kesi 239 zimeondolewa;

iii. Majalada 25 yamepokelewa kutoka ZAECA, majalada 2 yanaendelea na upelelezi, majalada 6 yalifungwa kwa sababu mbali mbali ikiwemo kukosa ushahidi na kuthibitisha tuhuma mahkamani, majalada 17 imeelekezwa yafunguliwe kesi Mahkamani;

iv. Majalada 131 kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar yamepokelewa ambapo majalada 86 yalipelekwa Mahkamani, majalada 7 yanaendelea na upelelezi. Majalada 11 yalipokelewa kutoka Jeshi la Polisi, majalada 8 yalifunguliwa kesi Mahkamani na majalada 3 yanaendelea na upelelezi;

v. Kesi 51 zimefunguliwa Mahkamani kati ya hizo kesi 9 zilizohusisha makosa ya kiuchumi na kesi 42 zilizohusisha Dawa za Kulevya. Aidha, kesi tatu ambazo zinahusu makosa ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi zilimalizika kwa mapatano ya kisheria ambapo washtakiwa walikubali kurejesha fedha na kulipa faini kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanyika. Kesi tatu zinazohusiana na uhujumu uchumi washtakiwa waliachiliwa huru. Kesi mbili za dawa za kulevya washtakiwa walipatikana na hatia na wanatumikia kifungo na kesi tatu ziliondoshwa Mahkamani kwa kukosekana ushahidi;

vi. Kanuni na miongozo 10 ya kimashtaka imeandaliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji katika masuala ya haki jinai;

vii. Vikao vya pamoja vimefanyika na wapelelezi, wachunguzi kutoka Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi - ZAECA, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – ZDCEA kwa lengo la kujadili changamoto zinazotokana na makosa ya

utakatishaji wa fedha haramu na hatua za kuchukuliwa kukabiliana na changamoto hizo;

viii. Uchunguzi wa pamoja kati ya Kikosi Kazi na Kituo cha Makosa ya Kiuchumi (Economic Crime Centre – ECC) umefanyika kwa kushirikiana na watendaji wa ndani na nje ya kituo kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa ushahidi toshelevu, sambamba na kuandaa kanzidata ya masuala ya kiuchunguzi kwa ajili ya kusaidia uwekaji taarifa muhimu;

ix. Waathirika watatu wa kesi za udhalilishaji walitembelewa na kupatiwa msaada wa kisaikolojia na hatimaye waliweza kutoa ushahidi Mahkamani; na

x. Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kimeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi 26 kutoka taasisi za Serikali katika maeneo mbali mbali ikiwemo mafunzo kuhusu sheria ya manunuzi; mafunzo ya uendeshaji wa mashtaka kwa taasisi zilizokasimiwa madaraka (Delegated Prosecution); na mafunzo ya usimamizi wa mikataba na taaluma ya uandishi wa nyaraka za kisheria (Legislative Drafting).

**59. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh. 5,636,600,000** (mishahara **Sh. 4,345,100,000 na Sh. 1,100,500,000** matumizi mengineyo) hadi Machi 2025 **Sh. 3,687,839,684** zimepatikana **(sawa na asilimia 65 ya lengo)** ambapo **Sh. 3,079,952,036** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 71 ya lengo)** na **Sh. 465,004,860** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 42 ya lengo).** Aidha, ruzuku ya **Sh. 190,400,000** imepangwa kutumika kwa uendeshaji wa Kituo cha Sheria, ambapo hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 142,862,788** zimepatikana **(sawa na asilimia 75 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).** Kituo cha Mafunzo ya Sheria na utafiti imepanga kukusanya **334,060,000.** Hadi kufikia Machi 2025, **Sh. 271,662,060** zimepatikana **(sawa na asilimia 81 ya lengo).**

### *2.3.5. Fungu G12: Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kishariah*

60. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imefanyiwa mapitio pamoja na Kanuni na Miongozo ya Mirathi, Wakfu na Hijja ili kukidhi mahitaji ya sasa;

ii. Tirka 945 mpya zimefunguliwa, tirka 1,027 zenye mali yenye thamani ya **Sh. 47,739,288,432** zimefungwa na warathi kupewa haki zao. Tirka 1,178 zinaendelea kushughulikiwa;

iii. Mashauri 75 ya mirathi yamepatiwa ushauri wa kisheria na mizozo 93 imepokelewa. Kati ya mizozo hiyo, 32 imepatiwa ufumbuzi, 49 inaendelea kushughulikiwa na 12 imepelekwa mahkamani kwa kutolewa hukumu;

iv. Wananchi 39 wameanza kuchangia Mfuko wa Hijja. Jumla ya **Sh. 16,000,000** na **US$ 2,000,** zimechangiwa;

v. Kamisheni imefanikisha utolewaji wa Zakka yenye thamani ya **Sh. 64,106,000** iliyotolewa na wazawa na familia kutoka Uturuki. Aidha, kwa kushirikiana na mashirika ya Muzdalifa, Direct Aid na wahisani wa Saud Arabia na UAE, imefanikisha kupatikana na kugawiwa misaada ya nguo, chakula, vifaa na fedha taslim yenye thamani ya **Sh. 2,494,500,000;**

vi. Nyumba 411 zimetunzwa na mashamba 14 yamesimamiwa na kupatiwa manufaa kwa kuzingatia wasia wa walioziweka wakfu na amana. Aidha, nyumba 7 zimefanyiwa matengenezo makubwa na 8 ya wastani. Matengenzo hayo yameghaarimu **Sh. 324,171,160;** na

vii. Katika uanzishaji wa miradi yenye tija jumla **Sh. 5,000,000,000** zimeekezwa Zanzibar Sukuk, na **Sh. 1,445,000,000** katika Mudharaba. Aidha, mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mayatima Tunguu chini ya ufadhili

wa taasisi ya *Vola World* ya Bahrain uko katika hatua za mwisho, na taratibu za kufanikisha miradi mikubwa ya ujenzi wa majengo ya na kilimo kwa hatua ya kwanza na ya pili zinaendelea.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 2,229,500,000** (mishahara **1,530,600,000** na **Sh. 698,900,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2025, **Sh. 1,406,121,511** zimepatikana **(sawa na asilimia 63 ya lengo),** kati ya fedha hizo, **Sh. 1,145,187,379** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 75 ya lengo)** na **Sh. 260,934,132** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 37 ya lengo).** Aidha, Kamisheni ilikadiriwa kukusanya mapato **Sh. 272,800,000,** hadi Mwezi Machi 2025 **Sh. 119,348,221** zimekusanywa **(sawa na asilimia 44 ya lengo). (Kiambatisho Nambari 1a na 1b)**

### *2.3.6. Fungu G14: Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu*

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mufti Mkuu. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Madrasa 276, Misikiti 95 na Maahad 2 zimekaguliwa katika maeneo ya Unguja na Pemba;

ii. Walimu wa madrasa 595 Unguja na Pemba wamehitimu mafunzo ya uwalimu na kupatiwa shahada na leseni za kufundishia. Kati ya hao, 250 wanaume na 345 wanawake. Mafunzo hayo yalifanyika katika maeneo tofauti. Aidha, wananchi 442 wamepewa vyeti vya uthibitisho wa kusilimu. Kati ya hao 335 ni wanawake na 107 ni wanaume;

iii. Migogoro 1,099 ya ndoa, talaka na mengineyo imepokelewa. Kati ya hiyo, 648 imetatuliwa, 88 imepelekwa mahkama ya kadhi, 2 imepelekwa ustawi wa jamii Pemba na 361 inaendelea kutafutiwa ufumbuzi;

iv. Mafunzo ya ndoa yameendelea kutolewa Unguja na Pemba, na wananchi 402 wamepatiwa mafunzo hayo (wanaume 165 na wanawake 237 - wakiwemo wawili 2 wenye mahitaji maalumu); na

v. Ofisi imefanikiwa kutoa mawaidha kuhusu kuimarisha amani na utulivu nchini katika misikiti ya Unguja na Pemba.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ilipangiwa kutumia **Sh. 2,295,300,000** (mishahara **Sh. 1,311,600,000** na matumizi mengineyo **Sh. 983,700,000).** Hadi Machi 2025, **Sh. 1,347,361,969** zimepatikana **(sawa na asilimia 59 ya lengo).** Kati ya fedha hizo, **Sh. 994,926,136** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 76 ya lengo)** na **Sh. 352,435,833** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 36 ya lengo). (Kiambatisho Nambari 1b).** Aidha, ruzuku ya matumizi mengineyo **Sh. 87,000,000** imepanga kutumika kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF). Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha zilizopatikana.

### *2.3.7. Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi*

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Fomu 2,856 za viongozi wa umma zimepokelewa na kusajiliwa (sawa na asilimia 112 ya makadirio). Kati ya Fomu hizo, Fomu 44 ziliwasilishwa nje ya muda. Aidha, Tume imeendelea kuchukuwa hatua za kisheria kwa viongozi waliochelewa kurejesha Fomu hizo;

ii. Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni umeendelea kuimarishwa kwa kupokea Fomu za Viongozi kwa kutumia Mfumo wa kielektroniki, na kupatiwa barua ya kupokelewa kwa njia ya kieletroniki na taarifa ya ujumbe mfupi kupitia simu ya kiongozi husika kujuulishwa kuwa fomu yake imepokelewa;

iii. Jumla ya viongozi wa umma 200 wamehakikiwa Unguja viongozi 176 na Pemba viongozi 24 (sawa na asilimia 87 ya makadirio);

iv. Malalamiko 23 ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya hayo, malalamiko 20 uchunguzi wake bado unaendelea kufanyika na malalamiko 3 uchunguzi wake umekamilika;

v. Ripoti ya 8 ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa Mwaka 2023/2024 imetayarishwa na kuwasilishwa sehemu husika;

vi. Elimu kuhusiana na maadili imetolewa kwa viongozi mbali mbali katika Taasisi na Serikali; na

vii. Maadhimisho ya Siku ya Maadili yamefanyika ambayo yameshirikisha Sekta ya Utawala Bora tarehe 10 Disemba,2024. Mgeni Rasmi katika kilele cha sherehe hiyo alikuwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kauli mbiu ***"Tudumishe Uzalendo kwa kukuza Maadili na Kuimarisha Utawala Bora kwa Maendelo ya Taifa".***

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Tume ilipangiwa kutumia **Sh. 1,948,300,000** (mishahara **Sh. 1,115,900,000** na **Sh. 832,400,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2025, **Sh. 1,186,625,941 (sawa na asilimia 61 ya lengo)** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh. 821,025,867 (sawa na asilimia 74 ya lengo)** zimetumika kwa mishahara na **Sh. 365,600,000 (sawa na asilimia 44 ya lengo)** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nambari 1b).**

### *2.3.8. Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma*

66. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Ofisi imefanya Ukaguzi wa hesabu za mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kukagua Wizara, Idara, Taasisi zinazojitegemea, pamoja na Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Mpango wa Ukaguzi "Audit Plan";

ii. Watumishi 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa upande wa Unguja na Pemba na watumishi 213 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi;na

iii. Ofisi imefanikisha utekelezaji wa Wiki ya Ukaguzi uliofanyika kuazia tarehe 13 hadi 18 Disemba, 2024 iliyokwenda sambamba na matukio tofauti yalioandaliwa na kutekelezwa.

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh. 7,823,300,000** (mishahara **Sh. 5,578,600,000** na matumizi mengineyo **Sh. 2,244,700,000).** Hadi Machi 2025, **Sh. 5,704,201,800 (sawa na asilimia 73 ya lengo)** zimepatikana. Kati ya fedha hizo**, Sh. 4,172,909,800 (sawa na asilimia 74 ya lengo)** zimepatikana kwa ajili ya mishahara na **Sh. 1,531,292,000 (sawa na asilimia 68 ya lengo)** zimepatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Ofisi ilikadiriwa kukusanya **Sh. 322,400,000.** Hadi Machi 2025, **Sh. 108,772,900 (sawa na asilimia 34 ya lengo)** zimekusanywa **(Kiambatisho Nambari 1a na 1b)**

### *2.3.9.Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.*

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Tuhuma 541 za makosa mbali mbali ya rushwa na uhujumu uchumi zimepokelewa zikiwemo kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya mali za umma na kukwepa kulipa kodi. Vile vile, majalada 25 yamefikishwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria na majalada 13 yamewasilishwa Mahkamani, Aidha, kesi 8 zimetolewa hukumu mahkamani, 2 zimeondolewa mahkamani, 3 zimekutwa na hatia Mahkamani na 3 hazikukutwa na hatia mahakamani;

ii. Mamlaka imeokoa na kudhibiti **Sh.17,196,564,608,** na **Dola za Kimarekani 33,441.** Kati ya fedha, **Sh.515,896,967** na **Dola 3,799** zimerejeshwa kwa wananachi na **Sh.16,680,667,641** na **Dola 29,642** zimerejeshwa Serikalini; na

iii. Mikutano 89 imefanyika katika Taasisi za binafsi na Taasisi za Serikali, mikutano 50 kupitia shehia, 57 semina, 23 uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa. Aidha, vipindi 17 vya radio na TV vimerushwa hewani.

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh. 6,259,900,000** (mishahara **4,928,300,000** na matumizi mengineyo **Sh. 1,331,600,000).** Hadi Machi 2025, **Sh. 3,362,515,674** zimepatikana **(sawa na asilimia 54 ya lengo)**. Kati ya fedha zilopatikana, **Sh. 2,576,013,955** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 52 ya lengo**) na **Sh. 786,501,667** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 59 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

### *2.3.10. Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma*

**70. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Kamisheni imepokea na kushughulikia mapendekezo ya Miundo ya Taasisi 6 na Miundo ya Utumishi 3 kutoka katika Taasisi mbali mbali za SMZ;

ii. Ripoti ya Mwaka ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imetayarishwa na kuwasilishwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.;

iii. Kamisheni imepokea na kutolea uamuzi rufaa 5 na lalamiko moja (1);

iv. Ziara ya kiutendaji katika Tume ya Utumishi wa Umma Tanzania Bara imefanyika. Lengo la ziara hiyo ni kubadilishana uzoefu katika ukusanyaji na uchambuzi wa Taarifa za Kiutumishi kwa kutumia mifumo ya kieletroniki; na

v. Elimu kwa jamii imetolewa kupitia vyombo vya habari kuhusu majukumu ya utumishi pamoja na majukumu ya Kamisheni.

**71. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamisheni ilipangiwa kutumia **Sh. 1,735,900,000** mishahara **Sh. 1,013,000,000** na matumizi mengineyo **722,900,000.** Hadi Machi, 2025, **Sh. 939,495,940 (sawa na asilimia 54 ya lengo)** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **746,666,366 (sawa na asilimia 74 ya lengo)** zimetumika kwa mishahara na **Sh. 192,829,500 (sawa na asilimia 27 ya lengo)** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nambari 1b).**

### *2.3.11. Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini*

**72. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Utumishi wa Serikalini. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Vibali vya ajira kwa watumishi 3,059 vimetolewa kwa Wizara na Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba. **(Kiambatisho Nambari 4)**;

ii. Watumishi 2,098 wamethibitishwa kazi, 647 wamepandishwa daraja, 205 wamebadilishwa kada, 16 wameidhinishiwa nyongeza ya muda wa utumishi na 166 ajira za mkataba. Aidha, Tume imeidhinisha

kustaafu kwa hiari watumishi 3, watumishi 425 wamestaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima, watumishi 13 wamestaafishwa kwa maradhi, likizo bila malipo imetolewa kwa watumishi 7 na kuacha kazi watumishi 7; na

iii. Tume imeidhinisha kufukuzwa kazi watumishi 10 baada ya kupatikana na makosa ya kinidhamu.

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii imepangiwa kutumia **Sh. 1,305,800,000** (mishahara **705,900,000** na matumizi mengineyo **599,900,000).** Hadi Machi 2025, **Sh. 787,067,608** zimepatikana, **(sawa na asilimia 60 ya lengo).** Kati ya fedha hizo, **Sh. 583,223,025** zimetumika kwa mishahara **(sawa na asilimia 83 ya lengo)** na **Sh. 203,846,500** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(sawa na asilimia 34 ya lengo) (Kiambatisho Nambari 1b).**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

74. **Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, imezingatia Mpango Mkakati wa Wizara 2024/2029, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021/2026, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Sera za Wizara na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2025 pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Kikanda na Kimataifa.

### *3.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, OR-KSUUB imepanga kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuendeleza matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Utumishi wa Umma;

ii. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Urithishaji Viongozi (Sussession Plan);

iii. Kukamilisha na kuendeleza Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mahkama

iv. Kuanza utekelezaji wa Mikataba ya Uwajibikaji kwa Viongozi (Performance Contracts);

v. Kuanzisha programu za mafunzo ya kujenga umahiri wa Watumishi wa Umma;

vi. Kuratibu na kusimamia masuala ya dini pamoja na mali za amana;

vii. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria mbali mbali;

viii. Kuendelea kuongeza uwelewa kwa jamii juu ya masuala ya msaada wa kisheria; na

ix. Kusimamia misingi ya utawala bora, maadili na kuongeza mapambano dhidi ya Rushwa pamoja na Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma.

### 3.2 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**76. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;

iii. Kusimamia na kuratibu Programu ya Utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma PSRP II;

iv. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali na kukuza uchumi;

v. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora, Uwajibikaji na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali; na

vi. Kuimarisha usimamizi wa udhibiti na rasilimali za Serikali.

### 3.3 Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**77. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha malengo ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Programu za Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

78. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatekeleza malengo yake kupitia mafungu ya bajeti 11 na Programu Kuu 14. Malengo ya utekelezaji kwa kila Fungu la Bajeti na Programu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni kama inavyowasilishwa hapo chini.

79. **Mheshimiwa Spika,** kati ya Programu hizi, Programu kuu nne (4) za fungu G01 zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu Kuu 11 zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

### *3.3.1 Fungu G01: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.*

80. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia Programu nne (4) na Taasisi mbili za ruzuku ambazo ni: -

#### *(i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria*

81. **Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa Programu hii, Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

   i. Kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria pamoja na kuendeleza utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

   ii. Kufanya ukaguzi na kutathmini kazi za watoaji msaada wa kisheria;

   iii. Kutoa elimu kwa jamii pamoja na kufanya mikutano ya masuala ya udhalilishaji kwa kushikiana na Watoaji Msaada wa Kisheria; na

   iv. Kuratibu na kushiriki vikao vya Katiba na Haki za Binadamu.

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara imepangiwa kutumi**a Sh. 348,975,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Sh. 85,000,000** ikiwa ni ruzuku kutoka kwa wahisani **(Kiambatisho Nambari 2).**

***ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora***

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kufanya tathimini ya utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji kazi wa Viongozi na Taasisi za Umma na kuwasilisha ripoti za tathmini katika Baraza la Mapinduzi;

ii. Kurusha hewani vipindi vya Utawala Bora, pamoja na masuala ya upatikanaji wa haki na utumishi kupitia televisheni mtandao (UB Online TV);

iii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mikataba ya Huduma kwa Mteja; na

iv. Kutayarisha Mpango wa kutathmini Taasisi za Umma kwa kutumia vigezo vya Utawala Bora.

**84.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepangiwa kutumika **Sh. 327,263,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

***(iii) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB***

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina maeneo mawili ya utekelezaji eneo la uendeshaji ambalo linatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na eneo la uratibu linalotekelezwa na Mipango, Sera na Utafiti.

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i Kutoa huduma za kiutumishi na stahiki za kiutumishi kwa watumishi wa Ofisi;

ii Kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, mfupi na mafunzo kwa vitendo; na

iii Kusimamia masuala ya uendeshaji wa Ofisi na kuweka mazingira bora ya kufanyiakazi.

**87. Mheshimiwa Spika,**Idara kwa Mwaka wa Fedha2025/2026, imepangiwa kutumia **Sh. 3,633,619,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2)**

**88. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i Kuratibu na kufanya mapitio na matayarisho ya Sera, Sheria, zinazosimamiwa na Ofisi;

ii Kuratibu utekelezaji wa mipango ya bajeti inayosimamiwa na Ofisi;

iii Kutayarisha Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Mpango wa Takwimu wa Wizara kwa lengo la kurahisisha ufuatiliaji na kupima kiwango cha ufanisi wa majukumu ya Ofisi;

iv Kuratibu na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zitakazowasilishwa Serikalini;

v Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria na Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Awamu ya Pili; na

vi Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Ofisi ikiwemo:

a) Mradi wa Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT);

b) Programu ya Upatikanaji wa Haki kwa WanawakenaWasichana katika Kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar; na

c) Programu ya Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria Awamu ya Pili.

89. **Mheshimiwa Spika,** programu hizi zitatekelezwa kupitia ufadhili wa Mashirika ya Maendeleo ambao ni UNDP, UN-Women, Ubalozi wa Uingereza, Uswisi na Umoja wa Ulaya.

90. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepangiwa kutumia **Sh. 412,782,500** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, Miradi inayosimamiwa na Ofisi imepangiwa kutumia **Sh.1,229,876,736** Mradi wa Upatikanaji wa Haki Kisheria, **Sh. 143,307,760** Mradi wa Uwezeshaji Wanawake na Wasichana katika kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar; **Sh.4,343,488,037** Mradi wa Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT); na **Sh. 1,500,000,000** Programu ya Mageuzi wa Sekta ya Sheria na Mageuzi ya Utumishi wa Umma Awamu ya Pili **(Kiambatisho Nambari 2).**

91. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Ofisi kwa upande wa Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na imepangiwa kutumia **Sh. 732,248,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

***(iv) Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.***

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma inatekelezwa na Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi pamoja Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma, Idara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:
    i Kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa Miaka Mitano 2025-2030;

    ii Kufanya mapitio ya Mpango wa Urithishwaji Madaraka, Mpango wa Rasilimali Watu na Mpango wa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo;

iii Kuandaa mifumo ya kieletroniki katika kuimarisha utoaji wa vibali vya ajira pamoja na kuandaa Mpango wa Rasilimali Watu;

iv Kufanya Uhakiki wa Tathmini ya mahitaji ya Mafunzo kwa Waizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali;

v Kufanya Mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu na Mpango wa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo; na

vi Kuratibu na kusimamia mafunzo ya aina zote (Cetralised Training Coordination System) kwa Watumishi wa Umma;

**94. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepangiwa kutumia **Sh. 1,309,843,420** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

**95. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hii kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi, imepanga kutekeleza yafuatayo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026: -

i. Kuandaa na kutekeleza Mkataba wa Viongozi wa Umma wenye kuleta matokeo na kutoa muongozo wake;

ii. Kandaa pamoja na Kufanya Utekelezaji wa Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi wa Kidijitali kwa Watumishi wa Umma;

iii. Kufanya Mapitio ya Miundo ya Taasisi kwa Kuzingatia Hati Idhini ya Serikali ili iweze kukidhi matakwa ya Wataka Huduma; na

iv. Kusimama utekelezaji wa Miundo ya Utumishi iliyofanyiwa mapitio itakayolenga upandishwaji wa vyeo kwa matokeo na sifa.

**96. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepangiwa kutumia **Sh. 894,569,200** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *(v) TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU*

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia Taasisi mbili zinazopokea ruzuku ambazo ni Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) na Skuli ya Sheria.

#### *a. Chuo Cha Utawala wa Umma*

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Cha Utawala wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya kuimarisha utendaji kazi kulingana na mahitaji yaliyopo katika Utumishi wa Umma;

ii. Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya Awali kwa waajiriwa wapya 1,000 wanaoingia katika ajira kwa mara ya kwanza;

iii. Kufanya Tafiti tatu katika Utumishi wa Umma ili kubaini mapungufu yaliyopo katika Utumishi na kuandaa programu za Mafunzo ya kujenga uwezo ili kuondooa mapungufu hayo; na

iv. Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya Muda mrefu kwa Watumishi wa Umma 244 na wananchi wengine 1,435 kutokana na mahitaji ya kiutumishi katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Chuo kimepangiwa ruzuku ya **Sh. 3,203,290,000** kwa ajili ya mishahara. **(Kiambatisho Nambari 2)**

#### *b. Skuli ya Sheria Zanzibar*

**100.** **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar kupitia Programu ya Mafunzo ya Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kutoa Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo kwa wahitimu wa fani ya sheria 70 kutoka Vyuo Vikuu katika ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Sheria;

ii. Kutoa Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo kwa wahitimu wa fani ya sheria 30 Kutoka Vyuo katika ngazi ya Stashahada ya Sheria (Mavakili);

iii. Kutoa Mafunzo ya kuwajengea uwezo wanasheria waliomo ndani na nje ya Serikali;

iv. Kutoa Mafunzo ya kuwajengea uwezo Waheshimiwa Majaji 13, Mahakimu 70, Makadhi 15, Mawakili, Wasaidizi wa Sheria pamoja na Watoa Msaada wa Kisheria; na

v. Kufanya utafiti kuhusiana na masuala ya kisheria.

**101. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Skuli ya Sheria imepangiwa kutumia Sh. 1,302,210,000 kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2)**

### *3.3.2 Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki- Mahkama Kuu Zanzibar*

**102. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuboresha mazingira na huduma za Mahkama;

ii. Kuimarishwa kwa upatikanaji wa Haki;

iii. Kuharakisha huduma za Mahkama na Usimamizi wa Mashauri;

iv. Kukuza imani na uelewa kwa jamii pamoja na hadhi ya Mahkama; na

v. Kuimarisha usimamizi wa utendaji, uhamasishaji wa rasilimali na uhusiano wa kimkakati na wahusika.

**103. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 66,389,200,000.** Kati ya hizo, **Sh.15,152,900,000** Mahkama Kuu, **Sh. 2,501,400,000** Mahkama ya Kadhi. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Mahkama imepangiwa kutumia **Sh. 48,600,000,000** ambapo **Sh. 13,000,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za

Mikoa na Wilaya, **Sh. 600,000,000** ni mchango wa Serikali katika uendeshaji wa Mradi wa Benki ya Dunia Zi - Jump. Aidha, Mahkama inatarajia kupata **Sh. 35,000,000,000** kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Zi – Jump.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mahkama imepangiwa kukusanya mapato ya **Sh. 1,277,267,000. (Kiambatisho Nambari 1a & 2).**

### *3.3.3 Fungu G03: Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**105. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha mfumo wa Sheria kwa kuandaa Kutayarisha, kuhifadhi na kusimamia masuala yanayohusu Uandishi wa sheria, Kanuni na Matangazo ya Kisheria;

ii. Kusimamia Mikataba, kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Maelewano (MoU);

iii. Kuendelea kuiwakilisha Serikali Mahkamani dhidi ya Kesi zote za Madai, kufuatilia indhari za kuishtaki Serikali;

iv. Kufanya uchambuzi na ushauri katika masuala mbali mbali ya Kesi za Madai;

v. Kushiriki katika mapatano pamoja Utekelezaji na Usimamizi wa Mikataba ya Serikali, Kikanda na Kimataifa; na

vi. Kufanya uchambuzi katika uandishi wa sheria, utafiti na mapitio ya Sheria za Zanzibar na kuzichapisha.

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu imepanga kutumia **Sh. 6,962,700,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *3.3.4 Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai-Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka*

107. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuimarisha miundombinu ya Ofisi kwa kujenga Ofisi mpya katika ngazi za mikoa na kukarabati zilizopo;

ii. Kushirikiana na Taasisi mbali mbali katika kutekeleza shughuli za kamati ya kuzuia udhalilishaji wa kijinsia na utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Haki Jinai;

iii. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na utendaji wa Ofisi;

iv. Kuimarisha kituo kwa ajili ya kuwajengea umahiri kwa waendesha mashtaka na wahusika wa sheria pamoja na kufanya tafiti; na

v. Kushirikiana na Taasisi mbali mbali za kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuwajengea uwezo waendesha mashtaka pamoja na kada ya utawala.

108. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 7,255,800,000** kwa matumizi ya kawaida. Aidha ruzuku ya **Sh. 228,600,000** imepangwa kutumika kwa ajili ya Kituo cha Utafiti wa Sheria. **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *3.3.5 Fungu G12: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah - Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana*

109. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuendeleza Miradi na Uwekezaji wenye Tija;

ii. Kuimarisha mifumo, Utendaji na huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na

iii. Kuimarisha mazingira ya Ofisi na utoaji wa huduma, kukamilisha mfumo wa kisheria, kimuundo na Utawala.

110. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii imepangiwa kutumia **Sh. 2,762,000,000** kwa matumizi ya kawaida. Aidha Kamisheni inatarajia kukusanya mapato ya **Sh. 336,222,000 (Kiambatisho Nambari 1a na 2).**

### *3.3.6 Fungu G14: Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini - Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar*

**111. Mheshimiwa Spika,** programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha utowaji wa fatwa, utafiti na usuluhishi wa migogoro;

ii. Kuimarisha elimu ya dini na kujenga mahusiano na taasisi za kidini; na

iii. Kukuza na kuimarisha utendaji wa shughuli za Ofisi; na

iv. Kuimarisha shughuli za kiislamu na kinga juu ya haki za wanawake na watoto.

**112. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 2,819,200,000** kwa kazi za kawaida **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *3.3.7 Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi-Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

**113. Mheshimiwa Spika,** programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma 2,500;

ii. Kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma;

iii. Kuendeleza Mfumo wa kieletroniki kwa usajili wa taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma;

iv. Kuelimisha viongozi wa umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili;

v. Kuendelea kuadhimisha kitaifa siku ya Maadili na Haki za Binaadamu; na

vi. Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu malalamiko na madai ya uvunjaji wa maadili ya viongozi wa umma.

**114. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 2,558,200,000** kwa matumizi ya kawaida **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *3.3.8 Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

**115. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i Kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya kukagua hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo Wizara, Mashirika na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi ya Maendeleo;

ii Kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar; na

iii Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali.

**116. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii imepangiwa kutumia **Sh. 8,837,200,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ofisi imepangiwa kukusanya mapato ya **Sh. 500,000,000. (Kiambatisho Nambari 1a na 2).**

### *3.3.9 Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.*

**117. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma (Public Expenditure Trucking Survery -PETS) katika miradi ya maendeleo ili kuimarisha ufanisi na kupata matumizi yanayoendana na thamani halisi ya miradi hiyo; na

ii. Kuendelea kuifuatilia jumla ya miradi 62 yenye thamani ya **Sh.1,795,189,696,441** na **USD 80,300,000,000.**

**118. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu imepangiwa kutumia **Sh. 10,871,800,000** kwa matumizi ya mishahara na mengineyo. Aidha, makusanyo ya

**Sh. 300,880,000** zinategemewa kukusanywa **(Kiambatisho Nambari 1a na 2).**

### *3.3.10 Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma – Kamisheni ya Utumishi wa Umma*

**119. Mheshimiwa Spika**, programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuendelea na kushughulikia Miundo ya Taasisi 8, Miundo ya Utumishi 8, kufanya ufualiaji wa miundo ya Taasisi 25 na Miundo ya Utumishi 25 iliyoidhinishwa na Serikali;

ii. Kukusanyaji wa taarifa za kiutumishi katika Utumishi wa Umma, kuangalia utekelezaji wa Muongozo wa Afya na Usalama Kazini jinsi unavyotekelezwa katika sekta ya Umma

iii. Kuendelea kufanya Ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 58, kufanya ukaguzi maalum katika Taasisi za Umma 20 Unguja na Pemba; na

iv. Kuandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2024/2025, kuratibu Mikutano itakayojadili masuala mbali mbali ya kiutumishi pamoja na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kiutumishi.

**120. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu imepangiwa kutumia **Sh. 1,811,300,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2).**

### *3.3.11 Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini – Tume ya Utumishi Serikalini*

**121. Mheshimiwa Spika,** programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i Kusimamia ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki;

ii Kusimamia haki na nidhamu za watumishi wa Serikali, kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi wasioridhika na uamuzi unaotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume;

iii Kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba 22, kuthibitisha kazi watumishi 3,242, kubadilisha kada watumishi 288, kupandisha daraja watumishi 980, kutoa nyongeza za muda wa utumishi 22, likizo bila ya malipo 15 na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali 985; na

iv Kutoa mafunzo ya uelewa kwa watumishi na waombaji ajira 1,467, kuimarisha huduma za kiutawala na za kiuendeshaji na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi watatu (3) na muda mfupi watumishi (2) wa Tume ya Utumishi Serikalini ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**122. Mheshimiwa Spika,** programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imepangiwa kutumia **Sh. 1,375,000,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2)**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 SHUKRANI NA HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

123. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, natoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wa maendeleo na taasisi zote za ndani zilizoshirikiana nasi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 katika kutekeleza majukumu yetu. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: - Jamhuri ya Watu wa China, Korea ya Kusini, India, Saudia Arabia, Oman, Ireland, Malaysia, Switzerland, Uingereza. Aidha, Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP), Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake (UN Women), Kituo cha Watoa Huduma za Kisheria (Legal Service Facility), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), 'BASEL Institute' na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

124. **Mheshimiwa Spika,** shukurani zangu maalum ziwaendee viongozi wenzangu katika Wizara na nikianza na Ndugu. Mansura Mosi Kassim, Katibu Mkuu, Ndugu. Mzee Ali Haji Naibu Katibu Mkuu (Katiba na Sheria), Ndugu. Omar Haji Gora, Naibu Katibu Mkuu (Utumishi na Utawala Bora), Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mtendaji Mkuu wa Mahkama na Warajis, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Naibu wake, Mkurugenzi wa Mashtaka na Naibu wake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Naibu wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mufti Mkuu na Kadhi Mkuu kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vizuri ya kusimamia utoaji wa haki na huduma kwawananchi.

125. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru, Wenyeviti wa Tume na Kamisheni, Makamishna na Wajumbe wote waliomo katika taasisi hizi, Wakuu wa Vitengo na Divisheni pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na taasisi zake kwa kuendelea kujituma kwa juhudi na maarifa katika kutekeleza malengo na majukumu ya Ofisi yetu. Niwaombe tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi na utoaji wa haki kwa wakati.

126. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, nawashukuru Taasisi zote za Kiraia zinazoshirikiana na Ofisi yangu, watoa Msaada wa Kisheria wote tunawapongeza kwa mashirikiano yao na moyo wao wa kujitolea. Watambue kwamba jitihada zao zina mchango mkubwa katika upatikanaji wa haki na Serikali inathamini juhudi zao.

127. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana nasi kwa karibu katika kutekeleza majukumu yetu. Juhudi zetu za pamoja ni muhimu katika kudumisha Muungano wetu.

128. **Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru wahusika wote wa Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao wametupatia ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza Sekta hii. Shukrani zangu za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote kwa kuchapa vizuri hotuba hii.

### 4.2 Hitimisho

129. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itaendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake yote muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu, kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kutoa

mchango mkubwa katika ukuaji wa demokrasia na uchumi wa nchi yetu.

130. **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Ofisi ya Rai - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake na malengo yalioelezwa katika hotuba hii, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Sh. Bilioni 131,337,472,653.** Kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 49,385,547,320** zitatumika kwa ajili ya mishahara, **Sh. 25,915,252,800** kwa ajili ya matumizi mengineyo **Sh. 220,000,000** ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka kwa wahisani, **Sh. 15,100,000,000** Miradi ya Maendeleo SMZ na **Sh. 40,716,672,533** Miradi ya Maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

131. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**MHESHIMIWA DKT. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar**

## 5.0 VIAMBATISHO

**Kiambatisho Nambari 1a: Makusanyo ya Mapato Julai/ Machi 2024/2025 na Makadirio ya Mwaka 2025/2026**

| IDARA/ TAASISI | Makusanyo ya Mapato Julai/ Machi 2024/2025 | | | Makadirio ya Mwaka 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|
| | **Makadirio** | **Makusanyo** | **%** | |
| Mahkama | 1,239,900,000 | 297,934,829 | **24** | 1,277,267,000 |
| **Jumla** | **1,239,900,000** | **297,934,829** | | **1,277,267,000** |
| Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 322,400,000 | 108,772,900 | **34** | 500,000,000 |
| **Jumla** | **322,400,000** | **108,772,900** | | **500,000,000** |
| Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi | | | | 300,880,000 |
| | | | | **300,880,000** |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 272,800,000 | 119,348,221 | **44** | 336,222,160 |
| **Jumla** | **272,800,000** | **119,348,221** | | **336,222,160** |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 3,243,805,000 | 1,412,834,842 | **44** | |
| **Jumla** | **3,243,805,000** | **1,412,834,842** | | |
| Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti | 334,060,000 | 271,662,060 | **81** | |
| **Jumla** | **334,060,000** | **271,662,060** | | |
| Skuli ya Sheria | 179,500,000 | 60,340,000 | **34** | |
| **Jumla** | **179,500,000** | **60,340,000** | | |
| **Jumla Kuu** | **5,592,465,000** | **2,270,892,852** | **41** | **2,414,369,160** |

**Kiambatisho Nambari 1b:Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha 2024/2025**

| MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA 2024/2025 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAM NDOGO** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOKADIRIWA** | **RUZUKU OC '000'** | **MISHAHARA** | **%SA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **%OC** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA** | **JUMLA FEDHA ZOTE (%)** |
| **Programu ya masuala ya kisheria** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa masuala ya kisheria | 202,791,520 | 120,000,000 | 322,791,520 | | 127,571,832 | 63 | 36,442,716 | 30 | **164,014,548** | **51** |
| **Jumla ya programu** | **202,791,520** | **120,000,000** | **322,791,520** | | **127,571,832** | | **36,442,716** | | **164,014,548** | |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utawala Bora | 184,168,720 | 119,200,000 | 303,368,720 | | 120,755,325 | 66 | 23,790,050 | 20 | **144,545,375** | **48** |
| **Jumla ya Programu** | **184,168,720** | **119,200,000** | **303,368,720** | | **120,755,325** | | **23,790,050** | | **144,545,375** | |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 1,838,050,196 | 1,550,000,000 | 3,388,050,196 | | 1,273,200,331 | 69 | 646,194,929 | 42 | **1,919,395,260** | 57 |
| Mipango,sera na utafiti | 250,376,480 | 150,000,000 | 400,376,480 | | 165,935,121 | 66 | 35,626,243 | 24 | **201,561,364** | 50 |
| Uratibu wa ORKSUUB-Pemba | 445,072,800 | 180,000,000 | 625,072,800 | | 280,541,902 | 63 | 81,000,000 | 45 | **361,541,902** | 56 |
| **Jumla ya Programu** | **2,533,499,476** | **1,880,000,000** | **4,413,499,476** | | **1,719,677,354** | | **752,821,172** | | **2,482,498,526** | **56** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa Umma** | | | | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 451,471,120 | 390,000,000 | 841,471,120 | | 334,575,295 | 74 | 79,596,260 | 20 | **414,171,555** | 49 |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 648,569,200 | 200,000,000 | 848,569,200 | | 504,489,114 | 78 | 34,239,460 | 17 | **538,728,574** | 63 |
| **Jumla ya Programu** | **1,100,040,320** | **590,000,000** | **1,690,040,320** | | **839,064,409** | | **113,835,720** | | **952,900,129** | 56 |
| **Jumla ya Programu-G01** | **4,020,500,036** | **2,709,200,000** | **6,729,700,036** | | | | | | **3,733,958,578** | **55** |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 3,191,100,000 | | 3,191,100,000 | | 2,263,071,202 | 71 | | | **2,263,071,202** | 71 |
| Skuli ya Sheria | 565,500,000 | 444,700,000 | 1,010,200,000 | | 450,656,315 | 80 | 270,266,756 | 61 | **720,923,071** | 71 |
| **Jumla ya Ruzuku - G01** | **3,756,600,000** | **444,700,000** | **4,201,300,000** | | **2,713,727,517** | | **270,266,756** | | **2,983,994,273** | 71 |
| **JUMLA KUU-G01** | **7,777,100,036** | **3,153,900,000** | **10,931,000,036** | | **5,520,796,437** | | **1,207,156,414** | | **6,717,952,851** | **62** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 7,849,900,000 | 4,586,100,000 | 12,436,000,000 | | 6,718,072,350 | 86 | 2,465,104,551 | 54 | 9,183,176,987 | 74 |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 1,485,600,000 | 479,100,000 | 1,964,700,000 | | 1,248,467,424 | 84 | 399,000,000 | 83 | 1,647,467,508 | 84 |
| **Jumla ya Programu G02** | **9,335,500,000** | **5,065,200,000** | **14,400,700,000** | | **7,966,539,774** | | **2,864,104,551** | | **10,830,644,325** | **75** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utoaji wa huduma za serikali | 3,543,100,000 | 2,369,600,000 | 5,912,700,000 | | 2,598,688,743 | 73 | 952,426,328 | 40 | 3,551,115,144 | **60** |
| **Jumla ya Programu G03** | **3,543,100,000** | **2,369,600,000** | **5,912,700,000** | | **2,598,688,743** | | **952,426,328** | | **3,551,115,144** | |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 4,345,100,000 | 1,100,500,000 | 5,445,600,000 | | 3,079,952,036 | 71 | 465,004,860 | 42 | 3,544,956,967 | 65 |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 190,400,000 | 190,400,000 | | | | 142,862,788 | 75 | 142,862,788 | 75 |
| **Jumla ya Programu G04** | **4,345,100,000** | **1,290,900,000** | **5,636,000,000** | | **3,079,952,036** | | **607,867,648** | | **3,687,819,684** | **65** |
| **Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah** | | | | | | | | | | |
| Uendeshaji na Usimamizi wa Wakfu, Hijja, Zakka na Mirathi | 1,530,600,000 | 698,900,000 | 2,229,500,000 | | 1,145,187,379 | 75 | 260,934,132 | 37 | 1,406,121,586 | **63** |
| **Jumla ya Programu - G12** | **1,530,600,000** | **698,900,000** | **2,229,500,000** | | **1,145,187,379** | | **260,934,132** | | **1,406,121,511** | |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Huduma za Serikali Mtandao** | | | | | | | | | | |
| Huduma za Serikali Mtandao | 1,541,000,000 | 2,154,800,000 | 3,695,800,000 | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Programu - G13** | **1,541,000,000** | **2,154,800,000** | 3,695,800,000 | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi na Uratibu wa Taasisi wa Taasisi na Masuala ya Kiisalmu | 1,311,600,000 | 983,700,000 | 2,295,300,000 | 87,000 | 994,926,136 | 76 | 352,435,833 | 36 | 1,347,362,045 | 59 |
| **Jumla ya Programu - G14** | **1,311,600,000** | **983,700,000** | 2,295,300,000 | | **994,926,136** | | **352,435,833** | | **1,347,361,969** | **59** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,115,900,000 | 832,400,000 | 1,948,300,000 | | 821,025,867 | 74 | 365,600,000 | 44 | 1,186,625,941 | 61 |
| **Jumla ya Programu - G15** | **1,115,900,000** | **832,400,000** | **1,948,300,000** | | **821,025,867** | | **365,600,000** | | **1,186,625,867** | **61** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 5,578,600,000 | 2,244,700,000 | 7,823,300,000 | | 4,172,909,800 | 75 | 1,531,292,000 | 68 | 5,704,201,875 | 73 |
| **Jumla ya Programu - E04** | **5,578,600,000** | **2,244,700,000** | **7,823,300,000** | | **4,172,909,800** | | **1,531,292,000** | | **5,704,201,800** | **73** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | | | | |
| Uzuiji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 4,928,300,000 | 1,331,600,000 | 6,259,900,000 | | 2,576,013,955 | 52 | 786,501,667 | 59 | 3,362,515,674 | 54 |
| **Jumla ya Programu - E05** | **4,928,300,000** | **1,331,600,000** | **6,259,900,000** | | **2,576,013,955** | | **786,501,667** | | **3,362,515,622** | **54** |
| | | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 1,013,000,000 | 722,900,000 | 1,735,900,000 | | 746,666,366 | 74 | 192,829,500 | 27 | 939,495,940 | 54 |
| **Jumla ya Programu - E07** | **1,013,000,000** | **722,900,000** | **1,735,900,000** | | **746,666,366** | | **192,829,500** | | **939,495,866** | **54** |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini** | | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 705,900,000 | 599,900,000 | 1,305,800,000 | | 583,223,025 | 83 | 203,846,500 | 34 | 787,069,608 | 60 |
| **Jumla ya Programu - E08** | **705,900,000** | **599,900,000** | **1,305,800,000** | | **583,223,025** | | **203,846,500** | | **787,069,525** | **60** |
| **JUMLA KUU** | **42,725,700,036** | **21,448,500,000** | **64,174,200,036** | **87,000** | **30,205,929,518** | | **9,324,994,573** | | **39,530,924,164** | **62** |

**Kiambatisho Nambari 1c: Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai/ Machi 2024/2025**

| MAPITIO 2024/2025 | | | | MUELEKEO 2025/2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **JINA LA MRADI** | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI** | **JUMLA** | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI** | **JUMLA** |
| Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria (LEAP II) | | 1,166,858,784 | **401,168,800** | | 1,229,876,736 | **1,229,876,736** |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (ZPSRP) | 1,000,000,000 | | **105,740,000** | 1,000,000,000 | | **1,000,000,000** |
| Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria | 500,000,000 | | **0** | 500,000,000 | | **500,000,000** |
| Mradi wa Upatikanaji wa haki kwa Wanawake na Wasichana katika kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar (UNWOMEN) | | 350,000,000 | **298,831,514** | | 143,307,760 | **143,307,760** |
| Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya | 25,500,000,000 | | **11,558,935,561** | 13,000,000,000 | | **13,000,000,000** |
| Mradi wa Maboresho ya Mahkama Zanzibar (Zi Jump) | | 28,500,000,000 | **7,821,652,550** | 600,000,000 | 35,000,000,000 | **35,600,000,000** |
| Mradi wa Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Mashauri | 500,000,000 | | **409,500,000** | 0 | - | |
| Mradi wa Kujenga Mpango Endelevu wa Kupambana na Rushwa (BSAAT - Z) | | | | | 4,343,488,037 | **4,343,488,037** |
| **JUMLA KUU** | **27,500,000,000** | **30,016,858,783** | **20,595,828,425** | | | **55,816,672,533** |

**Kiambatisho Nambari 2:Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| | KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI OC** | **JUMLA** | **RUZUKU OC** | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA KUU** |
| **Programu ya msuala ya kisheria** | | | | | | | |
| Usimamaizi wa masuala ya Kisheria | 126,183,000 | 222,792,000 | 348,975,000 | 85,000,000 | | | |
| **Jumla ya Programu** | **126,183,000** | **222,792,000** | **348,975,000** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | |
| Usimamzi wa Utawala Bora | 125,342,000 | 201,921,000 | 327,263,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **125,342,000** | **201,921,000** | **327,263,000** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 2,006,647,000 | 1,626,972,000 | 3,633,619,000 | | | | |
| Mipango,Sera na Utafiti | 255,053,000 | 157,729,500 | 412,782,500 | | 1,500,000,000 | 5,716,672,533 | **7,216,672,533** |
| Uratibu wa ORKSUUB-Pemba | 482,248,000 | 250,000,000 | 732,248,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **2,743,948,000** | **2,034,701,500** | **4,778,649,500** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa umma** | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 461,471,120 | 848,372,300 | 1,309,843,420 | | | | |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 684,569,200 | 210,000,000 | 894,569,200 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **1,146,040,320** | **1,058,372,300** | **2,204,412,620** | | | | |
| **Jumla ya Programu - G01** | **4,314,701,320** | **3,344,598,800** | **7,659,300,120** | | | | |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 3,203,290,000 | | 3,203,290,000.00 | | | | |
| Skuli ya Sheria | 679,810,000 | 622,400,000 | 1,302,210,000.00 | | | | |
| **Jumla ya Ruzuku-G01** | **3,883,100,000** | **622,400,000** | **4,505,500,000** | | | | |
| **JUMLA KUU** | **7,741,547,320** | **4,423,252,800** | **12,164,800,120** | **85,000,000** | **1,500,000,000** | **5,716,672,533** | **19,466,472,653** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 10,205,700,000 | 4,947,100,000 | **15,152,900,000** | 135,000,000 | 13,600,000,000 | 35,000,000,000 | |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 1,879,000,000 | 622,400,000 | **2,501,400,000** | | | | |
| **Jumla ya Programu - G02** | **12,084,700,000** | **5,569,600,000** | **17,654,200,000** | **135,000,000** | **13,600,000,000** | **35,000,000,000** | **66,389,200,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali | 3,632,900,000 | 3,329,800,000 | 6,962,700,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G03** | **3,632,900,000** | **3,329,800,000** | **6,962,700,000** | | | | **6,962,700,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 5,415,200,000 | 1,840,600,000 | 7,255,800,000 | | | | |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 228,600,000 | 228,600,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G04** | **5,415,200,000** | **2,069,200,000** | **7,484,400,000** | | | | **7,484,400,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Haki na Uwezeshaji Kishariah | 1,828,100,000 | 933,900,000 | 2,762,000,000 | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Programu - G12** | **1,828,100,000** | **933,900,000** | **2,762,000,000** | | | | **2,762,000,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | |
| Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya dini ya Kiislamu | 1,407,900,000 | 1,411,300,000 | 2,819,200,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G14** | **1,407,900,000** | **1,411,300,000** | **2,819,200,000** | | | | **2,819,200,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,209,400,000 | 1,348,800,000 | 2,558,200,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G15** | **1,209,400,000** | **1,348,800,000** | **2,558,200,000** | | | | **2,558,200,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 5,806,800,000 | 3,030,400,000 | 8,837,200,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E04** | **5,806,800,000** | **3,030,400,000** | **8,837,200,000** | | | | **8,837,200,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | |
| Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 8,473,700,000 | 2,398,100,000 | 10,871,800,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E05** | **8,473,700,000** | **2,398,100,000** | **10,871,800,000** | | | | **10,871,800,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 1,052,200,000 | 759,100,000 | 1,811,300,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu -** | **1,052,200,000** | **759,100,000** | **1,811,300,000** | | | | **1,811,300,000** |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **E07** | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 733,100,000 | 641,900,000 | 1,375,000,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E08** | **733,100,000** | **641,900,000** | **1,375,000,000** | | | | **1,375,000,000** |
| | | | | | | | |
| **JUMLA KUU** | **49,385,547,320** | **25,915,252,800** | **75,300,900,120** | **220,000,000** | **15,100,000,000** | **40,716,672,533** | **131,337,472,653** |

| Kiambatisho Nambari 3: Sheria Zilizofanyiwa Mapitio | |
|---|---|
| 1 | Sheria ya Utumishi wa Umma nam.2 ya mwaka 2011 katika eneo la upandishaji cheo (promotion) kwa watumishi wa umma. |
| 2 | Sheria ya Mahusiano Kazini nam.1 ya mwaka 2005 katika eneo la utatuzi wa migogoro ya wafanyakazi wa sekta binafsi, Eneo la biashara (kuangalia masuala ya wingi wa leseni na vibali kwa wafanyabiashara). |
| 3 | Sheria ya Umiliki wa Ardhi nam.12 ya mwaka 1992 |
| 4 | Sheria ya Usajili wa Ardhi nam.10 ya mwaka 1990 katika eneo la umiliki na usajili wa ardhi. |
| 5 | Sheria ya Mipango Miji na Vijiji Sura ya 85 ya mwaka 1955 katika eneo la mipango miji. |
| 6 | Sheria ya Maji nam.4 ya mwaka 2006 katika eneo la huduma na upatikanaji wa maji nchini. |
| 7 | Sheria ya Umeme nam.3 ya mwaka 2006 katika eneo la huduma na upatikanaji wa umeme nchini. |
| 8 | Sheria ya Uchaguzi nam.4 ya mwaka 2018 katika eneo la uchaguzi. |

| Kiambatisho Nambari. 4: Watumishi Walioajiriwa Kuanzia Julai, 2024 Hadi Machi, 2025 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NAM** | **WIZARA / TAASISI** | **WANAWAKE** | **WANAUME** | **JUMLA** |
| 1 | Wizara ya Afya | 667 | 397 | 1064 |
| 2 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 1273 | 469 | 1742 |
| 3 | Wizara ya Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora | 8 | 2 | 10 |
| 4 | Wakala wa Vipimo | 3 | 1 | 4 |
| 5 | Mamlaka ya Serikali Mtandao | 10 | 16 | 26 |
| 6 | Taasisi ya Elimu | 0 | 1 | 1 |
| 7 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale 57 (3) (a) | 1 | 4 | 5 |
| 8 | Ofisi ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 3 | 2 | 5 |
| 9 | Kamisheni ya Utalii 57 (3) (a) | 4 | 4 | 8 |
| 10 | Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu | 2 | 1 | 3 |
| 11 | Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar | 3 | 6 | 9 |
| 12 | Tume ya Utumishi Serikalini | 1 | 0 | 1 |
| 13 | Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi | 4 | 7 | 11 |
| 14 | Wizara ya Uchumi wa Buluu | 5 | 13 | 18 |
| 15 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 1 | 2 | 3 |
| 16 | Wizara ya Fedha na Mipango (Msajili wa Hazina) | 2 | 1 | 3 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 17 | Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais | 4 | 11 | 15 |
| 18 | Ofisi ya Mhasibu kuu | 48 | 22 | 70 |
| 19 | Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi | 2 | 4 | 6 |
| 20 | Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji | 8 | 9 | 17 |
| 21 | Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali | 6 | 4 | 10 |
| 22 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | 4 | 4 | 8 |
| 23 | Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi | 10 | 10 | 20 |
| **JUMLA** | | **2,069** | **990** | **3,059** |